

## **9:1-10:44 MATATIZO YA NDOA ZA MCHANGANYIKO**

### **Huzuni za Ezra (9:1-15)**

Tatizo mojawapo la kwanza lililomkabili Ezra lilikuwa lile la ndoa za mchanganyiko. Wanaume wa Israeli walikuwa wameoa wanawake wasiokuwa Waisraeli wakazaa nao watoto. Desturi ile ilienea sana hata kwa viongozi wa jumua, na kama ingeendelea hivyo ingeweza kuharibu dini ya Israeli na hata ukabila wao kuwa kabila la pekee (9:1-2).

Ezra alipoambiwa mambo hayo alijaa huzuni na aibu, akamgeukia Mungu na kuungama dhambi hiyo kwa niaba ya taifa lote (3-5). Alikubali kwamba Mungu alifanya haki alipowaadhibu watu wake mara nyingi kwa ajili ya uasi wao, akikubali wapelekwe kifungoni; lakini katika neema yake siku zote alibakiza baadhi yao ili kuendeleza taifa. Uhuru na ulinzi waliopewa na Waajemi wakati huo ulikuwa dalili nyingine ya neema ya Mungu (6-9). Hofu ya Ezra ilikuwa kwamba, kutokana na uasi wao kwa sheria yake, Mungu angeweza kuwaadhibu tena, lakini wakati huo asingeacha mabaki yo yote (10-15).

### **Matatizo yatatuliwa (10:1-44)**

Watu walipopata habari ya huzuni za Ezra, walikutana kwake pamoja na familia zao. Walikubali makosa yao na kuahidi kwa kiapo mbele yake kwamba wangeparekebisha (10:1-5). Lakini tatizo lililoenea kama hilo na lenye matokeo makubwa namna hiyo, halikuweza kutatuliwa siku moja tu. Kwa hiyo Ezra akaondoka kwenda faraghani katika chumba cha nyumba ya rafiki yake alipoweza kutafakari mbele ya Mungu usiku kucha kuhusu jambo hilo. Matokeo yake, mkutano mkubwa wa familia zote ulipangwa kuwepo baada ya siku tatu (6-8).

Siku ile ya mkutano hali ya hewa ilikuwa mbaya, lakini hata hivyo watu walikaa wakitetemeka katika baridi ya mvua ili wasikilize hukumu ya Ezra. Walikuwa na nia ya kweli ya kurekebisha maisha yao. Watu wachache tu walimnung'unikia Ezra alipotangaza kwamba wacosaji wawaondoe wake zao wa kigeni (9-15). Jambo lile lingechukua muda, kwa hiyo maafisa waliwekwa ili wasimamie mambo yote (16-17). Ndoa za mchanganyiko zilienea sana kwa viongozi wa dini na kwa watu wa kawaida pia, lakini mwishowe wote waliwaondoa wake zao wa kigeni. Pia walitoa sadaka kwa sababu ya dhambi zao (18-44).